HABARI NJEMA KWAKO

Dk. J. J. Robb F.R.C.P.

Imetafsiriwa na Douglas T.B. Mmari

Mara kwa mara maswali matatu hujitokeza kwenye mawazo ya watu, na si ajabu yanajitokeza. Kwa maana majibu yake ni ya maswali hayo muhimu sana.

Maswali hayo ni:

(a) Je, njia ya mbinguni ni katika msingi wa kifo cha Kristo pekee katika msalaba wa Kalvari miaka elfu mbili iliyopita na sisi tunahitaji kukubali hilo? Jibu la kiroho kwa swali hili ni “Ndiyo” pasipo shaka lolote.

(b) Je, njia ya mbinguni baada ya maisha ya hapa duniani inategemea msingi wa matendo yetu, jinsi tulivyofanya vibaya au vizuri wakati tukiwa duniani? Jibu la Biblia hapa ni “Hapana” na limetajwa bayana mara nyingi katika maandiko.

(c) Je, kuingizwa kwetu mbinguni siku moja ni matokeo ya jumlisho la jibu (a) na (b) hapo juu? Mwandishi hakufanikiwa kabisa kupata andiko ambalo linaunga mkono jibu la “Ndiyo” na hakuna yeyote aliyewahi kutoa hata moja, kwa ufahamu wangu.

Mwisho wa yote, ni kile ambacho neno la Mungu aliye hai, lisilokuwa na kosa linavyosema ndicho cha kutilia maanani, na sio maoni au ugunduzi wa mwanadamu yoyote au kundi la watu bila kujali jinsi wanavyoonekana waadilifu.

Barua ya Mtume Paulo kwa Wagalatia ni moja ya ushahidi wa kutumainika ambao tunaweza kuutegemea kwa ajili ya ukweli wa kimungu kuhusiana na majibu ya maswali yaliyoulizwa.

Kwa kujaribu kuelewa barua yoyote ni jambo la muhimu sana kujua angalau mambo matatu:

(a) Nani aliandika waraka huu?
(b) Kwa nini uliandikwa?
(c) Ni nani aliyeandikiwa?

Tunaweza kuwa na uhakika kuwa barua hii haikuandikwa ili kupoteza muda tu au kufurahisha. Paulo aliiandika akiwa na moyo uliojaa uzito na huzuni ambayo unaweza kuiona unaposoma kwa uangalifu.

Toleo la Biblia ya Habari Njema linatoa utangulizi mzuri na wa msaada mkubwa ambao ni vizuri kuutilia maanani wakati tunapotafakari kwa uangalifu yaliyomo katika barua.

Utangulizi unasomeka hivi: *Wakati habari njema kuhusu Yesu zilipoanza kuhubiriwa na kupokelewa na watu wasio Wayahudi swali lilijitokeza: "Je, ni lazima mtu aitii sheria ya Musa ili awe mkristo wa kweli?"*

Paulo anasema ya kuwa hili halikuwa muhimu. Ukweli pekee wa msingi wa maisha katika Kristo ulikuwa **IMANI** (katika Kristo) ambayo kwayo wote tunapatanishwa na Mungu.

Lakini katika baadhi ya makanisa ya Galatia, jimbo la Kirumi katika Asia Ndogo, palitokea watu waliompinga Paulo na kusema kwamba mtu anatakiwa pia kuitii sheria ya Musa ili aweze kupatanishwa na Mungu.

Barua ya Paulo kwa Wagalatia iliandikwa ili kurejesha tena imani na mwenendo wa kweli wa watu waliokuwa wakipotoshwa na mafundisho ya uongo.

Paulo anaanza kwa kutetea haki yake ya kuitwa mtume wa Yesu Kristo. Anasisitiza kuwa wito wake wa kuwa mtume

ulitoka kwa Mungu, na si kwa mamlaka yoyote ya kibinadamu na ya kuwa utume wake ulikuwa zaidi kwa wasio Wayahudi. Na ndipo anajenga hoja yake kuwa ni kwa **IMANI PEKEE** watu wanapatanishwa na Mungu.

Katika sura za kumalizia, Paulo anaonesha kuwa tabia ya kikristo hutokea kama matokeo ya upendo unaotokana na **IMANI KATIKA KRISTO**.

Paulo ndiye aliyeteuliwa kupeleka habari njema ya wokovu wa bure kwa mataifa na ndivyo alivyofanya. Petro ndiye angepeleka ujumbe kwa Wayahudi na hili alilifanya kwa uangalifu na kukawa na matokeo mazuri. Hata hivyo kazi hizi ziliingiliana kwa sehemu.

Petro alihubiri kwa Kornelio na nyumba yake ambayo ni ya watu wa Mataifa — angalia Matendo sura ya 10 kwa makini. Habari hii ya kushangaza na kuelekeza ni muhimu kujifunza.

Kwa upana zaidi, tungeweza kusema utume wa Paulo ulikuwa kwa Mataifa na wa Petro kwa Wayahudi.

Paulo akiongozwa na Mungu pasipo mashaka, alienda na kuhubiri ukweli kuhusu uharibifu wa mwanadamu. Uharibifu ulitokana na anguko katika bustani ya Edeni, na matokeo ya kusikitisha tunayaona kila siku popote tulipo. Aliwaeleza wanadamu pia **habari njema** ya wokovu wa bure kwa kutubu dhambi zao kwa Mungu na kumpokea Kristo. Kazi yake ILIYOKAMILIKA pale msalabani ilitosha kabisa kukutana na mahitaji yao ya ndani na kuwafanya wafae kwenda mbinguni.

Wagalatia walipokea ukweli huo ambao hata sasa ni hivyo, unaendana na neno la Mungu lisilo na kosa wala kubadilika.

Yote yalienda sawa kwa muda na Wagalatia walikuwa na furaha. Kisha wakatokea watu, si kwamba walimwonea Paulo wivu tu bali pia walifuatilia mahali alipoenda. Bila shaka watu hawa walishawishiwa na shetani. Walijitahidi kuwashawishi Wagalatia ya kwamba, pamoja na mambo yote kuwa sawa lakini iliwapasa watahiriwe (Wagalatia 5:2-6), na kuheshimu hili kwa kutii sheria yote (amri za Mungu) ili kukamilisha wokovu (angalia Wagalatia 1:6-9 na 3:1-13).

Paulo anaandika kupinga jambo hili na kusahihisha kosa ambalo wanaweza kuliamini. Anawahakikishia kwa kurudia tena na tena kuwa wokovu na uzima unaofaa kuingia mbinguni ni katika msingi wa kifo cha Kristo pekee na sisi tukikubali pasipo na matendo.

Hakika kutahiriwa pekee hakuna maana yoyote. Ilikuwa ni kile tu inachomaanisha. Kwa kweli hakuna hata mmoja aliyewahi kutimiza amri zote (isipokuwa Kristo). Kulikuwa na zaidi ya amri kumi. Lakini hata kutimiza kumi ilikuwa ni vigumu mno kwa binadamu aliyeanguka. Na unajua, tunahitaji kuvunja kiungo kimoja tu, ili kukata mnyororo wote. Wote tuna mnyororo uliokatika.

Yakobo 2:10 *"Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote."*

Hakuna mtu awezaye kubadili neno la Mungu, kwa kutumia ujanja au jitihada kubwa. Kila waliojaribu kujitahidi kufanya hivyo iliwagharimu sana.

Inashangaza jinsi ambavyo kila sehemu ya neno la Mungu linavyosimama au kuanguka kwa pamoja. Kila sehemu inaunga mkono habari yote, na habari yote inaunga mkono kila sehemu.

Bwana Yesu Kristo ndiye pekee aliyeweza kushika amri zote. Aliitukuza sheria na kuifanya iheshimike (Isaya 42:21).

Watu waliompinga Paulo huenda walikuwa ni wayahudishaji kutoka Yerusalemu. Watakuwa walipinga yote aliyofundisha Wagalatia, lakini walijua hawakuwa na tumaini la kufanikiwa katika hilo.

Kama nilivyotangulia kusema kuwa, tangu Paulo alipompokea Kristo pale kwenye barabara ya Dameski, alikuwa na watu waliompinga katika yale yote aliyoyafanya kwa ufanisi kwa ajili ya Mwokozi na Bwana wake. Inawezekana mwishoni walimwuua.

DHAMBI

Kwa sababu ya anguko la wazazi wetu wa kwanza katika Bustani ya Edeni kila mwanadamu aliyezaliwa katika dunia tangu wakati ule (isipokuwa Kristo) amezaliwa mwenye dhambi. Hivyo, amekufa kiroho, na anahitaji uzima ambao unapatikana katika Kristo pekee na wokovu wake mkuu (Waebrania 2:3) bila kujali wana uzima kiasi gani kimawazo na kimwili. Waraka wa Paulo kwa Warumi unaeleza hili bila makosa kwa uwazi na upana *(angalia hasa Warumi sura ya 3).*

Hii haikuwa barua ya kwanza Paulo kuandika; Wagalatia na Wathesalonike zilikuwa ni nyaraka za kwanza kuandikwa kwa kusudi jema sana.

Mungu, akiwa Mungu wa utaratibu na anayetawala yote, alipanga kuwa Waraka kwa Warumi uwe wa kwanza katika

Biblia. Lazima tusome na tuelewe ukweli wa Warumi kabla hatujakubali kwa undani ukweli katika nyaraka zingine.

Katika Warumi, sura ya kwanza mataifa wana hatia, wameanguka na kuzama katika dhambi. Kwa hakika hawawezi kufanya lolote linaloweza kuwapa upendeleo wa Mungu.

Katika Warumi 2:1-3 wanafiki wana hatia na wamezama. Anajaribu kuwashawishi wengine kwa mambo yale ambayo hata yeye anahukumiwa.

Kabla hatujaenda katika Warumi 3, tunaona Waebrania (yaani Wayahudi) hawaamini na hivyo wana hatia licha ya upendeleo wa kipekee walio nao.

Sura hiyo hiyo inatujulisha bila mashaka kuwa wanadamu wote (ulimwengu wote) wana hatia mbele za Mungu (Warumi 3:19) – kwamba kila kinywa kitanyamazishwa na ulimwengu wote utakuwa una hatia mbele za Mungu.

Itaonekana kama "ulimwengu wote" umewekwa katika nyumba ya hukumu ya Mungu, na uko kizimbani. Ushahidi unatolewa, hakuna la kujitetea, hukumu inatolewa – **ANA HATIA**

Warumi 3:9-10 *"Ni nini basi? Tu bora kuliko wengine? La! Hata kidogo. Kwa maana tumekwisha kuwashitaki Wayahudi na Wagiriki ya kwamba pia wamekuwa chini ya DHAMBI. Kama ilivyoandikwa ya kwamba, hakuna mwenye haki hata mmoja."*

(Tafadhali soma Warumi 3 ili upate picha ya kweli.) Pamoja na hayo Mungu ana njia ya kutuokoa katika Mwanawe na kifo chake cha kulipia dhambi. Kifo chake kinatosha sana

kwa hitaji la ndani na kumfanya mwanadamu astahili kuingia mbinguni kwa masharti mepesi kabisa.

Waefeso 2:1-3 *"Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu, ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi; ambao zamani, sisi sote nasi tulienenda kati yao, katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwili na ya nia, tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira kama wengineo wote."*

Warumi 3:23 *"Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."*

Lazima tupate picha kamili katika mawazo yetu na tujue kwa hakika ni wapi na kwa jinsi gani tunasimama mbele za Mungu mtakatifu. Kama vile tutakavyoweza kuonekana mbele za ndugu zetu haina umuhimu sana, na kwa kweli haipasi. Kwa kweli hali ya uharibifu wa mwanadamu haiwezi kulinganishwa na mpango wa wokovu wa Mungu upatikanao katika nafsi ya Mwana wake. Maandiko yanasemaje – Warumi 10:8-11.

Hili ndilo jambo la kutilia maanani ambalo Paulo na Petro walilihubiri kila mahali walipoenda. Limeandikwa wazi kwa ajili yetu katika neno la Mungu lisilo na kosa.

Mungu alibariki huduma yao, wengi waliongozwa kwa Yesu kwa wokovu na mara wakafaa kuingia mbinguni na bila shaka siku itakapofika itadhihirika.

Paulo alisema katika 1 Korintho 2:2, "*Maana niliazimu nisijue neno lolote kwenu ila Yesu Kristo, na yeye aliyesulubiwa".*

Hii inahusisha hatia kisha neema katika njia ya ajabu ya wokovu unaotolewa kama tukikubali.

"Alibeba pale mtini
Hukumu kwa ajili yangu
Na sasa mdhamini
Na wenye dhambi wako huru."

Ni wazi kuwa hili lilimgharimu Mungu kilicho bora zaidi mbinguni, Mwanawe wa pekee na ilimgharimu Mwanawe uhai wake katika hali ya mateso yasiyoelezeka. Na faida kubwa inatolewa bure kwa yeyote atakayekubali kupokea. Ufunuo 22:17.

Ni jambo la kufurahisha kwamba kabla Biblia haijafika mwishoni, huruma ya Mungu inatoa nafasi ya mwisho wa wokovu kwa yeyote anayehitaji na yuko tayari kupokea upendeleo wa bure.

Katika Ufunuo 22:17 maji ya uzima ni wokovu wa Mungu, hati ya kusafiria kwenda mbinguni kutoka katika ulimwengu ulioharibika, na mambo yaliyo mazuri zaidi – *tazama Waebrania 6:9*.

Kwa nini awaye yeyote akose hilo? Hakuna anayetaka kupotea. Wote wanaweza kuishi milele kwa sababu Kristo alikufa. Bora zaidi, wokovu haubadiliki. Mwokozi alisema katika Yohana 10:28, *"Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea* ***kamwe****".*

Katika kifungu hiki anaongea juu ya kondoo wake. Yeye ndiye anayewatunza – Yuda 24, Yohana 17:11-12, Zaburi 121:5.

Katika maandiko matakatifu, ile hali ya mtu kutambua hitaji la wokovu na kumpokea Kristo kama Mwokozi, ni hatua ya

kwanza ya njia ya mbinguni, na kwa kweli ni tendo la kwanza tunaloweza kufanya ambalo litampendeza Mungu.

Warumi 8:8 *"Wale waufuatao mwili* (hiyo ni kama walikuwa wamezaliwa katika ulimwengu huu) ***HAWAWEZI KUMPENDEZA MUNGU****."*

Mtu mmoja aliyejulikana na mwandishi alikuwa na nia kubwa kuona ustawi wa milele wa nafsi za wengine. Akiwa na wazo hili, alikuwa anaweka karatasi nyuma ya bahasha ya baadhi ya barua zilizotumwa na shirika. Wazo lilikuwa kila mtu ambaye ujumbe huu utampitia, na hasa yule aliyekuwa mlengwa, wangesoma na kutilia maanani ujumbe uliomo. Ujumbe huo ulisomeka kama ifuatavyo:

"Nafasi hapa ingepotea bure,
Lakini tangu nilipoionja
Furaha ya neema ya ajabu ya Mungu
Nitawapasha habari
Jinsi ambavyo Kristo kutoka katika utukufu
Alikufa kwa ajili ya kizazi maskini kilichoanguka.
Alijali sana hadi
Dhambi zenu alizibeba

Alipotundikwa katika mti wa Kalvari.
Sasa anaishi milele
Na amesimama kwenye mlango wako
Akingoja tu awe Mwokozi wako."

Mskoti aliyejulikana sana na mwandishi alifurahia sana wimbo huu mfupi. Alikuwa na sauti ya kupendeza, alikuwa mwimbaji bora na kumsikia akiimba hakika ingekufurahisha. Maneno yake ni ya kweli na yanayovutia kama ifuatavyo:

Mara niliposikia sauti katika moyo wangu wenye giza
Nikaamshwa katika usingizi wa dhambi
Ilikuwa ni Yesu aliyegonga, kabla aliwahi kugonga
Sasa nikasema 'Bwana mbarikiwa, karibu ndani.'

Kiitikio:
Kisha fungua, fungua, fungua, mruhusu Bwana aingie,
Kwa sababu moyo utang'aa kwa nuru ya mbinguni,
Ukimruhusu Bwana aingie.

Wimbo huu mdogo unahusiana na mlango wa moyo wa mwanadamu. Mwana wa Mungu aliyekufa kwa ajili ya kila mmoja wetu, anataka kuingia, kubadili maisha yetu na kutupa utoshelevu. Kuna eneo katika moyo wa mwanadamu ambalo ni Mungu na Kristo tu wanaweza kulijaza. Alilitengeneza kwa ajili yake na anahitaji kuingia. Ingekuwa vema kwa msomaji kukubali kumruhusu hata leo.

Mtume Petro aliandika mambo mazuri ya thamani ambayo yamekuwa ya baraka kwa watu wengi hata baada ya yeye kuondoka. Hakika maandiko yake yote yalikuwa na mamlaka ya juu kabisa.

1 Petro 3:18 ni mmoja wa mstari wa kipekee na wenye mwongozo wa kipekee: *"Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu; akauawa kimwili, lakini akahuishwa kiroho."*

Inawezekana msomaji ulikwisha soma mstari huu mara nyingi. Unaweza kufafanuliwa kama ifuatavyo, na hivyo kudhihirisha maana yake ya kupendeza:

"Kwa maana **Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi**."

Hiki ni **KIPATANISHO au TULIZO.** Hiki kinamaanisha kuwa ni mahali pa kukutana ambapo Mungu aliyekosewa anaweza kuja na kukutana na mwenye dhambi aliyemkosea, na kumsamehe dhambi zake zote, za wakati uliopita, za sasa na za siku zijazo.

"Mungu hawezi kumpita mwenye dhambi,
Sheria yake inamdai kuwa inampasa kufa.
Kisha kwenye msalaba wa Kristo ninaona
Jinsi Mungu anavyoweza kuokoa
Na kuendelea kuwa mwenye haki."

Unaona katika msalaba wa Kalvari deni lote lililipwa kabisa na Mungu kwa neema yake kuu. Anapenda kukutana na mwenye dhambi hapo na sio kumsamehe tu bali kumhesabia haki – yaani kumwacha kama mtu ambaye hajawahi kutenda kabisa dhambi. Kumbuka kwamba hilo linategemea hiari ya mtu wala hakutakuwa lazima.

Warumi 5:1 *"Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika **IMANI**, na muwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo."*

"**Mwenye haki kwa ajili ya wasio haki**"

Hii ni **MBADALA**. Yeye hakuwa na dhambi kabisa, mwenye haki wakati sisi hatukuwa wenye haki kabisa. Bila kujali tunawaza nini, mwenye haki aliingia katika hatia ya mwenye dhambi, akateseka badala yake.

"Mwujiza mkuu wa NEEMA:
Kwa ajili ya mwanadamu Mwokozi alimwaga damu."

Kristo alitosheka na hili na kusema “IMEKWISHA”. Mungu alipendezwa na kuthibitisha kutosheka kwake wakati alipomfufua Mwanawe kutoka katika wafu.

Kama wewe msomaji hutosheki na tendo hili kwa nini usifanye hivyo? Kuna aliye juu au mkuu kuliko Mungu na Kristo?

“***Ili atulete kwa Mungu***”

Huu ni **UPATANISHO**. Wakati mwanadamu alipoacha kumtii Mungu na kutenda dhambi, ilileta utengano mkuu. Mungu alimfukuza mwanamume na mkewe kutoka katika bustani (Mwanzo 3:24).

Mwanadamu amekuwa nje tangu wakati huo, lakini Mungu anataka kumrudisha kwake – UPATANISHO.

Ilikuwa kwa gharama kubwa, iliyolipwa kwa ukamilifu, Mungu alitoa bure kupitia wokovu mkuu, msamaha, amani na Mungu, kuhesabiwa haki, furaha mbinguni na nyumbani milele kwa yeyote na wote watakaompokea Kristo kama Mwokozi na Bwana (Yohana 1:12).

Matendo 13:39 inasema: *“Na kwa yeye kila amwaminiye huhesabiwa haki katika mambo yale yote <u>asiyoweza kuhesabiwa haki</u> kwa Torati ya Musa”*

Kitu ambacho sheria ingeweza kufanya ni kuonyesha dhambi, kumhukumu mwenye dhambi, na kumwacha akiwa bila msaada wowote na bila tumaini (Warumi 7:7-13).

Warumi 3:20 “*Kwa maana kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria* (amri).”

Sheria haiwezi kwenda zaidi ya hapo. Inatuachia hapo. Hata hivyo ni nzuri kwa sababu inatuonyesha hali yetu halisi na uhitaji wetu wa ndani, kama tuna hekima ya kutazama njia itoshayo ya ukombozi wetu.

Ukombozi huu uko tayari na unatosha kutuliza haja ya mwenye dhambi nyingi na kumtayarisha afae kwa ajili ya mbinguni:

> *"Je? Umesoma jinsi alivyomwokoa mnyang'anyi aliye-kuwa anakufa*
> *Alipokuwa ametundikwa juu ya mti*
> *Aliyetazama kwa macho ya huruma na kusema,*
> *Eh! Bwana unikumbuke."*

Maombi yake yalijibiwa wakati ule ule bila matendo. Kwa sababu hakuwa na hata tendo moja, wala hakuwa na muda wa kuwaza kufanya hayo.

Unaweza kusoma habari hii katika Luka 23:39-43.

Mnyang'anyi mwingine alikuwa na nafasi ile ile lakini ina-onesha alikufa bila kutubu na baadaye – aliingia UMILELE.

Sasa turudi kwenye 1 Petro 3:18. "*Akauawa kimwili*," hapa tuna mambo mawili **KUFANYIKA MWILI** na **KUSULUBISHWA.**

Kwanza **KUFANYIKA MWILI**

Mwana wa Mungu kama Mungu hakuweza kufa. Alipewa na kupokea mwili wa kibinadamu usio na dhambi. Hili alifanya na alikufa kwa hiari, akautoa uhai wake baada ya mateso makali. Hakuna mtu ambaye angeweza kuuchukua kutoka kwake. Anatuambia hivyo katika Yohana 10:18, *"Hakuna mtu aniondoleaye, bali mimi nautoa mwenyewe. Nami ninao uweza wa kuutoa, ninao uweza wa kuutwaa tena."*

“Damu ya kafara ikawa lazima imwagike
Mchungaji huyu kwa uchungu aliongozwa
Kusimama kati yetu na adui
Na kwa hiari yake akafa badala yetu.”

Akauawa kimwili

Hii ni **KUSULUBISHWA**.

“Walimgongea Bwana wangu misumari juu ya mti
Wakamwacha hapo akifa,
Kwa kupitia upendo alikufa pale kwa ajili yangu,
Ulikuwa upendo usiolinganishwa na chochote.”

NEEMA ya ajabu, UPENDO upitao wote, uchungu usioelezeka, hata hivyo bado kuna wengine wanaosema haitoshi. Wanasema, lazima tufanye sehemu yetu kumsaidia, vinginevyo mpango wake utashindwa. Hili ni vigumu kuelewa kwa mtazamo wa lile ambalo Mungu anasema katika neno lake takatifu.

“**Lakini akahuishwa kiroho**”

Huu ni **UFUFUO.** Mungu Baba alipendezwa na kazi ambayo Mwanawe aliifanya pale msalabani kwa niaba yetu, ili iwe dhabihu ya mara moja na kwa wakati wote, kwamba alimfufua katika wafu na kumweka katika mkono wake wa kuume kule mbinguni.

“Hii ndiyo dhabihu aliyotoa
Sheria ya Mungu haingedai zaidi ya hapo
Kwa sababu hakuna hata senti ambayo haikulipwa
Alipochukua hukumu yangu.”

Tukiangalia ukweli wote huu, ingekuwa kwetu hekima ya kufanya sehemu rahisi tu anazotuambia tuzifanye:

(a) Kubali kuwa hatia yetu, hitaji letu
na kushindwa kwetu kabisa kutimiza hitaji hilo.

(b) Amini yale anayosema.

(c) Inua macho yako kwake
na umwone akichukua adhabu yetu.

(d) Mpokee kama Mwokozi na Bwana wetu.

Yohana 3:36 *"Amwaminiye Mwana* ***ana*** *(*sasa*) uzima wa milele; asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia."*

Kama nafasi ingekuwepo ya kupoteza uzima huu, usingekuwa uzima wa **MILELE** tuliopata. **MILELE** ina maana inadumu **MILELE**. Milele ni hali isiyogeuzika na isiyo na mwisho na milele yatufikisha salama kwenye utukufu wa daima.

Ukumbuke kwamba mwisho wa mstari huu unasema: *"asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia."*

Kumwamini kunaleta wazo la kumtegemea kabisa na kile alichokifanya kikamilifu na hivyo kutotegemea jitihada zetu zisizokuwa na mafaniko. Hivyo hakuna mwanadamu yeyote anayeweza kufanya chochote cha kumpendeza Mungu au kukubalika naye.

Tayari imetajwa katika Warumi 8:8, *"Wale waufuatao mwili hawawezi* ***kumpendeza Mungu****."* Wanahitaji kuzaliwa upya kiroho.

Yesu alisema katika Yohana 3:3,7, *"Hamna budi kuzaliwa mara ya pili."* Na alimaanisha yale aliyosema.

Matendo yanayofanywa kwa Bwana baada ya kuokoka yatapata ujira mbinguni, lakini kwa njia yoyote si cheti cha kuingia mbinguni.

Maandiko yanaweka bayana kuwa wokovu ni kwa NEEMA pekee kwa njia ya IMANI.

IMANI ni sawa na kusema: Ninaacha yote na ninamtegemea na kumpokea Yeye – au kukataa na kulipa gharama.

Waefeso 2:5 *"Tumeokolewa kwa NEEMA."*

Waefeso 2:8 *"Kwa maana mmeokolewa kwa NEEMA, kwa njia ya IMANI; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu."* NEEMA ni upendeleo wa Mungu tusiostahili.

NEEMA ni sawa na kusema: Mungu ndiye mwanzilishi wake (Tito 2:11), Neema ikomboayo, iliyo tele (1 Timotheo 1:14). Neema ya Kristo (2 Korintho 8:9), inadumu milele.

Tukipata zawadi, je, tuna haja ya kuifanyia kazi? Ni kweli hatuhitaji.

Waefeso 2:9 *"Wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu."*

Warumi 4:4 *"Lakini kwa mtu afanyaye kazi, ujira wake hauhesabiwi kuwa ni NEEMA bali kuwa ni deni."*

Hii ina maana gani? Kuna baadhi ya watu ambao hawayajui vema maandiko kama wanavyotakiwa. Wanafikiri kwamba wanaweza kuufanyia kazi wokovu wao katika maisha yao, na kumweka Mungu kuwa mdeni wao, kiasi kwamba atawalipa na mahali pale mbinguni mwisho wa maisha yao mafupi. Wamekuwa wajinga mno. Hakuna mwanadamu anayeweza kumweka Mungu kuwa na DENI. Kila mmoja anadaiwa na Mungu pigo linalofuata la moyo wake, pumzi inayofuata, chakula kinachofuata, kwa kweli kwa kila kitu kinachofuata. Mungu anaweza na kweli ndivyo anavyofanya mara kusitisha kila kitu ghafla au kwa wakati wowote. Ni nini kinachofuata baadaye? UMILELE.

Waefeso 2:5 *"Tumeokolewa kwa NEEMA."*

Warumi 4:5 *"Lakini kwa mtu asiyefanya kazi, bali ANAMWAMINI yeye ambaye amhesabia haki asiyekuwa mtauwa, imani yake mtu huyo imehesabiwa kuwa haki."* Hii itakuwa ya kushangaza.

Warumi 3:24 *"Wanahesabiwa haki BURE kwa NEEMA yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu."*

Wagalatia 2:16 *"Lakini tukijua ya kuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, bali kwa IMANI ya Kristo Yesu; sisi tulimwamini Kristo Yesu ili tuhesabiwe haki kwa imani ya Kristo, wala si kwa matendo ya sheria; maana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki."*

Tito 2:11 *"NEEMA ya Mungu iwaokoao wanadamu wote imefunuliwa."*

Warumi 11:6 *"Lakini ikiwa ni kwa NEEMA, haiwi kwa matendo tena, au hapo NEEMA isingekuwa NEEMA."*

Katika kitabu cha “Safari ya Msafiri” yule mtu mwenye mzigo mgongoni mwake alipofika msalabani na kuona kile kilichotendeka pale, mzigo wake ulianguka mgongoni mwake. Alipoendelea kuuangalia ukiwa unabingirika bondeni na asiuone tena ndipo alipoongozwa kwa kusema: *“Usifiwe msalaba, lisifiwe kaburi. Linalozidi yote: asifiwe Mwokozi.”*

“Ananiambia maneno ambayo kwayo nimeokoka.
Ananionyesha jambo ambalo LIMEFANYWA TAYARI,
Alilikamilisha katika mlima wa Kalvari
Kwa njia ya Mwanawe mpendwa,
Ambaye kwake matendo yangu hayana nafasi,
la sivyo NEEMA pamoja na matendo si NEEMA tena.”

Kuna **mafungu manne** mafupi ya maneno muhimu:

Amosi 4:12 *“Ujiweke tayari kuonana na Mungu wako.”*
Maneno ya **USHAURI MWEMA**.

Yohana 3:3,7 – Yesu anasema: *“Hamna budi kuzaliwa mara ya pili.”*
Maneno yenye **MAMLAKA YA JUU KULIKO YOTE**.

2 Wakorintho 5:20 *“Mpatanishwe na Mungu.”*
Maneno yenye **WITO WA KWELI**.

1 Wakorintho 15:3 *“Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu.”*
Maneno ya **MWITIKIO RAHISI**.

Msingi imara pekee tunaopaswa kujenga juu yake – dhambi zote zimegongomelewa msalabani (Wakolosai 2:14). Na hivyo hakuna kitu kitakachotuzuia kuingia mbinguni. Dhambi zinatufungia mlango wa kuingia mbinguni, lakini sasa zinaondolewa kama tunaamini na kuupokea ukweli huu.

Mathayo 11:28 ni mstari mzuri na wa thamani sana kwa sababu nyingi, hasa kwa kuwa ni Mwokozi, ni Mwana wa Mungu mwenyewe aliyesema. Maneno yake yanatuhusu hadi leo:

“Njoni kwangu*, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.”*

“Njoni kwangu” – **Inaonesha jinsi anavyotutunza na kutujali.**

“Wote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo” – **Inaonesha aina ya watu anaowaalika.**

“Nami nitawapumzisha” – **Faraja anayotoa**

NJONI – **Tendo linalotakiwa kufanywa**

KWANGU – **Mahali tunapoongozwa kuelekea**

Je, Mwokozi, Bwana na Mungu anatimiza ahadi yake au anaweza kuivunja?

“Pumzika katika msamaha na tulizo
Kutoka katika mzigo wa hatia na huzuni
Pumzika katika damu ikomboayo
Pumzika katika amani timilifu ya Mungu.
Wewe, dhabihu iondoayo dhambi

Una thamani sana machoni pangu
Wewe pekee utakuwa pumziko langu
Sasa na hata MILELE.”

Tukiwa tumefika huko tunaweza kufanya kitu chochote kinachoweza kukubalika mbele za Mungu. Tendo lolote hata kama lingekuwa zuri na la kupendeza halitaweza kutuingiza mbinguni au hata kusaidia, kwa sababu linategemea **kabisa** kazi aliyoimaliza Kristo pale msalabani. Na kazi yetu ni kukubali hayo bila kusita na kudumu katika hayo.

Hata hivyo, pale mbinguni furaha itakamilika mahali pale pazuri pasipoelezeka kwa maneno baada ya kukaguliwa na hakimu wa haki – Mungu mwenyewe ambaye hafanyi kosa lolote.

Mbinguni ni mahali pa milele, pasipofananishwa na popote duniani.

Waefeso 2:7 inazungumzia *"Zamani zinazokuja."*

Si kwa muda wa miaka tu bali kwa MILELE.

Ukiwa na maswali zaidi unaweza kutuandikia.
Agiza somo la kwanza la Emmaus Shule ya Biblia
bure kutoka kwa

Emmaus Shule ya Biblia kwa njia ya Posta
S.L.P. 1330
Moshi

Emmaus Shule ya Biblia kwa njia ya Posta
S.L.P. 1424
Dodoma